



**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania**

# **Takwimu za Mawasiliano**

**Robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024**

**[www.tcra.go.tz](http://www.tcra.go.tz)**

ISO 9001: 2015 CERTIFIED

Toleo 1.0

## Kuhusu ripoti hii

Ripoti hii inawasilisha takwimu za mawasiliano za robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa ujumla, ripoti inatoa takwimu za mawasiliano ya simu, pesa mtandao, Intaneti, utangazaji, posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto, na huduma nyingine zinazohusiana na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Takwimu zimeandaliwa kulingana na viwango vya Umoja wa Mawasiliano Duniani (ITU) vya kukusanya na kuandaa takwimu za huduma za mawasiliano/TEHAMA.

## Yaliyomo

<b>1</b>	<b>Takwimu za Mawasiliano ya Simu</b>	<b>1</b>
1.1	Idadi ya laini za Simu	1
1.2	Bei za huduma za mawasiliano ya simu	5
1.3	Huduma ya sauti ya mawasiliano ya simu	9
1.4	Idadi ya ujumbe mfupi wa maneno (SMS)	13
1.5	Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu	15
1.6	Idadi ya minara ya mawasiliano ya simu	17
1.7	Idadi ya mitambo ya kurushia mawimbi ya simu	18
<b>2</b>	<b>Takwimu za Pesa Mtandao</b>	<b>20</b>
2.1	Akaunti za pesa mtandao	20
2.2	Idadi ya miamala ya pesa mtandao	21
<b>3</b>	<b>Takwimu za Huduma ya Intaneti</b>	<b>22</b>
3.1	Laini za Intaneti	22
3.2	Matumizi ya mwezi ya huduma ya Intaneti	24
3.3	Uwezo wa kiunganishi cha Intaneti kimataifa	24
3.4	Usimikaji na kasi ya huduma ya Intaneti	25
3.5	Idadi ya Vikoa vya Intaneti	26
<b>4</b>	<b>Takwimu za Huduma za Utangazaji</b>	<b>27</b>
4.1	Visimbuzi vilivyolipiwa	27
4.2	Idadi ya visimbuzi vilivyouzwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita	28
4.3	Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya	29
4.4	Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita	30
4.5	Ueneaji wa huduma za utangazaji	30
<b>5</b>	<b>Takwimu za Huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto (Courier)</b>	<b>31</b>
5.1	Idadi ya masanduku ya posta	31
5.2	Wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto	31
5.3	Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi	31
5.4	Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi	32
5.5	Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka ndani ya nchi	33
5.6	Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi	33
5.7	Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani na nje ya nchi kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita	34
5.8	Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi na kupokelewa kutoka nje ya nchi	35
<b>6</b>	<b>Ubora wa Huduma, Ufuatiliaji wa Masharti ya Leseni na Majaribio ya Ulaghai Mtandaoni</b>	<b>36</b>
6.1	Ubora wa huduma za simu na Intaneti	36
6.2	Ufuatiliaji wa masharti ya leseni ya utangazaji	44
6.3	Ubora wa huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto	47
6.4	Majaribio ya ulaghai	48
<b>7</b>	<b>Idadi ya Leseni na Vyeti</b>	<b>51</b>
7.1	Leseni	51
7.2	Vyeti	52
<b>8</b>	<b>Hitimisho</b>	<b>53</b>

# 1. Takwimu za Mawasiliano ya Simu

Takwimu za mawasiliano ya simu kuhusu usajili, bei, dakika za mawasiliano, ujumbe mfupi (SMS) na vifaa vya mawasiliano zimeainishwa kwa mwezi, robo mwaka na mwaka.

## 1.1. Idadi ya laini za simu

Sehemu hii inahusika na laini za simu za mkononi na za mezani ambazo zimetumika kwenye huduma ya mawasiliano angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita. Kuna aina mbili za laini: zinazotumika kwa mawasiliano ya binadamu (Person to Person - P2P) na zinazotumika kwa mawasiliano ya mashine (Machine to Machine - M2M).

Jumla ya idadi ya laini (P2P na M2M) zilizosajiliwa imeongezeka kutoka milioni 76.6 katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024 hadi milioni 80.7 kwa robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024. Hilo ni ongezeko la asilimia 5% kama inavyoonekana hapo chini.

Kufikia Juni 2024

**Milioni 76.6**

Kufikia Septemba 2024

**Milioni 80.7**



**5.4%**

### 1.1.1 Idadi ya laini za P2P

**75.6  
Milioni**

Kufikia Juni  
2024



**79.6  
Milioni**

Kufikia Septemba  
2024



**5.4%**


Laini za simu za mkononi na mezani zilizosajiliwa kwa ajili ya P2P kwa kila mtoa huduma katika robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024 zimeoneshwa kwenye Jedwali 1.1.1.

### Jedwali 1.1.1 Idadi ya laini za simu za mkononi na mezani za P2P zilizosajiliwa kwa kila mtoa huduma

	Airtel	Halotel	Tigo	TTCL	Vodacom	Jumla
Julai	19,349,803	10,288,681	22,234,092	1,718,668	23,402,345	76,993,589
Agosti	19,533,663	10,598,149	22,836,771	1,574,711	23,657,084	78,200,378
Septemba	19,492,734	10,971,582	23,458,325	1,586,724	24,136,856	79,646,221

Takwimu katika Jedwali 1.1.1 zinaonesha ongezeko la wastani kwa kila mwezi wa 1.7% ya laini za simu za mkononi na mezani ndani ya robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024.

### 1.1.2 Idadi ya laini za simu kwa ajili ya M2M kwa kila mtoa huduma



Jedwali 1.1.2 linaonesha laini zilizosajiliwa kwa mawasiliano ya M2M kwa robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024.

**Jedwali 1.1.2 Idadi ya laini za M2M zilizosajiliwa**


	Airtel	Halotel	Tigo	TTCL	Vodacom	Jumla
Julai	328,576	57,430	43,100	6,515	559,877	995,498
Agosti	330,069	58,563	47,615	4,496	566,361	1,007,104
Septemba	331,676	59,913	48,539	4,495	571,197	1,015,820

### 1.1.3 Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma


Chati 1.1.3a na 1.1.3b zinaonesha mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma. Takwimu za P2P kwa ujumla zinaonesha kuna ushindani wenye tija kati ya watoa huduma.

Hata hivyo, kwa usajili wa M2M, Vodacom anaongoza ikiwa na 56.2% ya laini zote zilizosajiliwa kama inavyoonekana kwenye Chati 1.1.3b. Airtel inashika nafasi ya pili kwa 32.7%, ikifuatiwa na Halotel kwa 5.9%.

**Chati 1.1.3a Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma wa P2P**



**Chati 1.1.3b Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma wa M2M**



### 1.1.4 Idadi ya laini za simu za mkononi na mezani

Jedwali 1.1.4 linaonesha idadi ya laini za simu za mkononi na mezani, na laini za M2M zilizosajiliwa kwa kipindi kinachoishia Septemba 2024.


**Jedwali 1.1.4 Idadi ya laini za simu za mkononi na mezani, na laini za M2M**

	Simu za mkononi	Simu za mezani	Laini za M2M	Jumla
Julai	76,915,542	78,047	995,498	77,989,087
Agosti	78,122,181	78,197	1,007,104	79,207,482
Septemba	79,568,173	78,048	1,015,820	80,662,041

### 1.1.5 Mabadiliko ya idadi ya laini za simu kwa kila mtoa huduma


Kulikuwa na ongezeko la laini za P2P katika robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024 la takriban milioni 4. Chati 1.1.5a inaonesha mabadiliko ya idadi ya laini za P2P kufikia Septemba 2024.

**Chati 1.1.5a Mabadiliko ya idadi ya laini za simu za P2P kwa kila mtoa huduma**



Aidha, kulikuwa na ongezeko la idadi ya laini za M2M katika robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024 la laini 46,380. Chati 1.1.5b inaonesha mabadiliko ya idadi ya laini za M2M kufikia Septemba 2024.

**Chati 1.1.5b Mabadiliko ya idadi ya laini za simu za M2M kwa kila mtoa huduma**




### 1.1.6 Idadi ya laini za simu kwa kila mkoa

Idadi ya laini za simu za mkononi na mezani, na M2M kwa kila mkoa imeoneshwa kwenye Chati 1.1.6. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2024/2025, Dar es Salaam ilishika nafasi ya kwanza kwa kuwa na laini milioni 14.8, Mwanza ilishika nafasi ya pili kwa kuwa na laini milioni 5.3, Arusha ilishika nafasi ya tatu kwa kuwa na laini milioni 4.9, Mbeya ilishika nafasi ya nne ikiwa na laini milioni 4.6, na Dodoma ilishika nafasi ya tano kwa kuwa na laini milioni 4.3.


Mikoa yenye laini chache zilizosajiliwa katika robo ya kwanza ya 2024/2025 ni Kaskazini Unguja yenye laini 73,743 Kusini Unguja yenye laini 110,970, na Kusini Pemba yenye laini 124,472.

### Chati 1.1.6 Idadi ya laini za simu za mkononi na mezani kwa kila mkoa

#### Tanzania Bara



#### Zanzibar



### 1.1.7 Idadi ya laini za simu katika kipindi cha miaka mitano iliyopita

Mwenendo wa idadi ya laini za simu kwa ajili ya mawasiliano ya P2P kwa miaka mitano iliyopita hadi 2023 umeoneshwa katika Jedwali 1.1.7.


**Jedwali 1.1.7 Idadi ya laini za simu kwa miaka mitano iliyopita**

	2019	2020	2021	2022	2023
Simu za mkononi	47,685,232	51,220,233	54,044,384	60,192,331	70,215,144
Simu za mezani	76,288	72,469	71,834	84,696	75,732
<b>Jumla</b>	<b>47,761,520</b>	<b>51,292,702</b>	<b>54,118,218</b>	<b>60,277,027</b>	<b>70,290,876</b>
<b>Asilimia ya Ueneaji</b>	<b>78%</b>	<b>81%</b>	<b>88%</b>	<b>98%</b>	<b>111%</b>

Takwimu katika Jedwali 1.1.7 zinaonesha ongezeko la laini za simu kwa wastani wa 10% kwa mwaka na ongezeko la wastani wa kiwango cha kusambaa (penetration) kwa laini za simu miongoni mwa watu cha 9% kwa mwaka. Kiwango hicho kilifikia 111% mwishoni mwa Disemba 2023, ikimaanisha kuwa kwa kila wakazi 10 kulikuwa na laini 11 kwa ajili ya huduma za mawasiliano ya simu.

### 1.2 Bei za huduma za mawasiliano ya simu

Sehemu hii inawasilisha wastani wa bei nje ya vifurushi (Basic tariff) na ndani ya vifurushi (Bundle tariff) kwa huduma za sauti, SMS ndani ya nchi, Afrika Mashariki (EA) na mataifa mengine (RoW), na data.



Mabadiliko ya bei nje ya vifurushi kwa robo ya mwaka iliyoishia Juni na Septemba 2024 yameoneshwa kwenye Jedwali 1.2.

**Jedwali 1.2 Mabadiliko ya bei (Tsh) za mawasiliano ya simu**

	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	Afrika mashariki (EA)	Mataifa mengine (RoW)	SMS kitaifa	SMS kimataifa	Data
Juni 2024	26.00	28.00	713.16	1,869.45	7.80	189.61	9.35
Septemba 2024	26.00	28.00	696.68	1,948.22	7.80	189.61	9.35
<b>Badiliko</b>	<b>0%</b>	<b>0%</b>	<b>-2%</b>	<b>4%</b>	<b>0%</b>	<b>0%</b>	<b>0%</b>

Kama inavyooneshwa katika muhtasari hapo juu, wakati bei za kupiga simu ndani na nje ya mtandao, SMS kitaifa (local SMS), SMS kimataifa na data hazikubadilika, bei za kupiga simu za Afrika Mashariki zilipungua kwa 2% na mataifa mengine ziliongezeka kwa 4%.



## 1.2.1 Bei za huduma ya sauti

Bei za huduma ya sauti kwa robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024 kwa simu za ndani na nje ya nchi zimeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.1. Hizi ni bei za sauti kwa dakika moja wakati mtumiaji anapiga simu ya ndani au ya kimataifa bila kujisajili kwenye kifurushi.

### Jedwali 1.2.1 Bei (Tsh) za kupiga simu ndani na nje ya nchi kwa kila mtoa huduma

Mtoa huduma	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	EA	RoW
Airtel	30.00	30.00	614.40	1,426.60
HALOTEL	10.00	20.00	875.00	1,565.00
TIGO	30.00	30.00	1,030.00	1,673.33
TTCL	30.00	30.00	217.60	2,871.33
VODACOM	30.00	30.00	746.40	2,204.83
<b>Wastani</b>	<b>26.00</b>	<b>28.00</b>	<b>696.68</b>	<b>1,948.22</b>

Jedwali 1.2.1 linaonesha kuwa watoa huduma wote hutoza Tsh 30 kwa dakika ndani na nje ya mtandao, isipokuwa Halotel inayotoza Tsh 10 kwa dakika ndani ya mtandao na Tsh 20 nje ya mtandao. Wastani wa bei ya huduma ya sauti ndani ya mtandao katika robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024 ilibaki sawa na robo ya mwaka inayoishia Juni 2024.

Aidha, Jedwali 1.2.1 linaonesha kuwa bei ya huduma ya sauti kimataifa zilitofautiana baina ya watoa huduma. Wastani wa bei ya huduma ya sauti kwa dakika moja kwa Afrika Mashariki na nchi nyingine ni Tsh 696.68 na 1,948.22, mtawalia.

## 1.2.2 Bei za SMS na data

Bei bila kifurushi nje na ndani ya nchi kwa SMS na data hadi Septemba 2024 zimeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.2.

### Jedwali 1.2.2 Bei (Tsh) za SMS na data

Mtoa huduma	SMS ndani ya nchi	SMS nje ya nchi	Data/Mb
Airtel	8	215.00	9.35
Halotel	5	95.00	9.35
Tigo	8	215.00	9.35
TTCL	10	138.06	9.35
Vodacom	8	285.00	9.35
<b>Wastani</b>	<b>7.8</b>	<b>189.61</b>	<b>9.35</b>

Wastani wa bei za SMS kitaifa (Tsh 7.80), SMS nje ya nchi (Tsh 189.61) na data (Tsh 9.35) kwa Septemba 2024 ulibaki kama ilivyokuwa kwenye robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024.

### 1.2.3 Bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi

Bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi kwa dakika moja ya sauti, SMS moja na MB moja ya data kwa watumiaji waliojiunga na kifurushi zimeoneshwa hapo chini.

#### Jedwali 1.2.3a Mabadiliko ya bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi

Kipindi	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	SMS	Data
Julai - Sept 2024	4.75	6.34	1.47	2.17
Apr - Juni 2024	4.66	6.18	1.42	2.16
<b>Badiliko</b>	<b>1.9%</b>	<b>2.5%</b>	<b>3.3%</b>	<b>0.3%</b>

Kielelezo hapo juu kinaonesha kuwa bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi zimebadilika katika robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024 ikilinganishwa na robo ya mwaka inayoishia Juni 2024. Bei za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao, na SMS ziliongezeka kwa viwango tofauti kama ilivyooneshwa kwenye kielelezo hapo juu.

Jedwali 1.2.3b linaonesha kuwa wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu katika kifurushi ziko chini kuliko bei za huduma za mawasiliano ya simu bila kifurushi kama inavyooneshwa katika jedwali 1.2.1.

#### Jedwali 1.2.3b Bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi

Mtoa huduma	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	SMS	Data
Airtel	4.19	7.04	1.58	2.05
Halotel	3.02	4.76	1.00	2.16
Tigo	4.67	6.61	1.28	2.06
TTCL	7.48	7.48	2.26	2.26
Vodacom	4.39	5.80	1.21	2.32
<b>Wastani kwa Sekta</b>	<b>4.75</b>	<b>6.34</b>	<b>1.47</b>	<b>2.17</b>

Wastani wa bei za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandano, kwa Sekta imeongezeka hadi Tsh 4.75 na Tsh 6.34 kwa dakika, mtawalia, katika robo mwaka inayoishia Septemba 2024, kutoka Tsh 4.66 na Tsh 6.18 katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024.

### 1.2.4 Wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu

Wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu ndani na nje ya kifurushi umeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.4.

#### Jedwali 1.2.4 Wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu kwa Sekta

	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	SMS	Data
Wastani bila kifurushi	26.00	28.00	7.80	9.35
Wastani katika kifurushi	4.75	6.34	1.47	2.17

Jedwali 1.2.4 linaonesha kuwa wastani wa bei za huduma ya mawasiliano ya simu bila kifurushi ni karibu mara tano zaidi ya wastani wa bei katika kifurushi na hivyo kupelekea watumiaji wengi (99.9%) kupendelea kujiunga na huduma za vifurushi.

## 1.2.5 Wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, mwenendo wa wastani wa bei za huduma za sauti na SMS nje ya vifurushi kwa Sekta, kitaifa na kimataifa umeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.5a, 1.2.5b na 1.2.5c.

### Jedwali 1.2.5a Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za sauti nje ya vifurushi kwa miaka mitano iliyopita

	2019	2020	2021	2022	2023
Ndani ya mtandao	149.00	57.00	34.00	32.00	29.00
Nje ya mtandao	189.00	57.00	34.00	32.00	30.00

Jedwali la 1.2.5a linaonesha kuwa wastani wa bei za huduma za sauti nje ya vifurushi kwa dakika ndani na nje ya mtandao zilipungua kati ya mwaka 2019 hadi Disemba 2023. Aidha, gharama hizo zililingana kuanzia mwaka 2020 hadi Disemba 2022. Ulinganifu huo ulisababishwa na kushuka kwa gharama za muingiliano wa mawasiliano ya simu za sauti (interconnection charges) baina ya watoa huduma.

### Jedwali 1.2.5b Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za sauti kimataifa nje ya vifurushi kwa miaka mitano iliyopita

	2019	2020	2021	2022	2023
EA	770.00	830.00	966.00	1,103.00	1,171.00
RoW	1,357.00	1,379.00	1,564.00	1,817.00	1,776.00

Jedwali 1.2.5b linaonesha kuwa kuna mienendo tofauti ya wastani wa bei za huduma za sauti kimataifa kutokana na viwango vya tozo za huduma za mawasiliano vinavyowekwa na watoa huduma wa kimataifa (international carriers).

### Jedwali 1.2.5c Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za kutuma SMS kitaifa na kimataifa nje ya vifurushi kwa miaka mitano iliyopita

	2019	2020	2021	2022	2023
SMS kitaifa	36.00	20.00	13.00	11.00	11.00
SMS kimataifa	160.00	176.00	172.00	193.00	200.00

Pia, katika kipindi cha miaka minne iliyopita mwenendo wa wastani wa bei za huduma za mawasiliano katika vifurushi umeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.5d.

### Jedwali 1.2.5d Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi katika kwa miaka minne iliyopita

	2020	2021	2022	2023
Ndani ya mtandao	9.38	7.84	7.27	4.90
Nje ya mtandao	11.21	8.69	7.78	6.30
SMS	3.45	3.35	2.69	1.37
Data	1.73	1.61	1.86	2.14

### 1.3 Huduma ya sauti ya mawasiliano ya simu

#### 1.3.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi

Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao nchini kwa robo ya mwaka inayoishia Juni 2024 na Septemba 2024 imeoneshwa hapo chini.

Kufikia Juni 2024

**Bilioni 39.6**

Kufikia Septemba 2024

**Bilioni 41.1**



**4%**

Kielelezo hapo juu kinaonesha kuongezeka kwa idadi ya dakika za huduma za sauti ndani ya nchi kwa 4% katika robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024.

**Dakika ndani ya mtandao**



**-1%**

Robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024

**Bilioni 21.3**

Robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024

**Bilioni 21.1**

**Dakika nje ya mtandao**



**10%**

Robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024

**Bilioni 18.2**

Robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024

**Bilioni 20.0**



Jedwali 1.3.1 linaonesha kuwa Julai 2024 ulikuwa mwezi wenye idadi ya dakika nyingi zaidi ikilinganishwa na miezi mingine ya robo ya mwaka huo.

#### Jedwali 1.3.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao nchini


	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	Jumla
Julai	7,188,565,697	6,907,084,322	14,095,650,019
Agosti	7,009,335,392	6,683,441,109	13,692,776,501
Septemba	6,890,640,823	6,442,809,635	13,333,450,458
<b>Jumla</b>	<b>21,088,541,912</b>	<b>20,033,335,066</b>	<b>41,121,876,978</b>

Jedwali 1.3.1 linaonesha takriban dakika bilioni 41.1 zilitumika katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2024 ikilinganishwa na dakika bilioni 39.6 katika robo mwaka iliyoishia Juni 2024. Hata hivyo, idadi ya dakika ndani ya mtandao ilikuwa kubwa zaidi ikilinganishwa na nje ya mtandao katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024.

### 1.3.1.1 Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti ya ndani na nje ya mtandao nchini

Mgawanyo wa dakika ndani na nje ya mtandao nchini umeoneshwa kwenye Chati 1.3.1.1a.


#### Chati 1.3.1.1a Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao




Chati 1.3.1.1a inaonesha kuwa dakika nyingi za sauti nchini zilitumika kwenye simu za ndani ya mtandao (51.3%) kuliko simu za nje ya mtandao (48.7%). Aidha, takwimu zinaonesha kuwa watu walipendelea zaidi kupiga simu ndani ya mtandao mmoja kuliko kupiga nje ya mtandao.

Mgawanyo wa dakika ndani na nje ya mtandao nchini kwa kila mtoa huduma umeoneshwa kwenye Chati 1.3.1.1b na 1.3.1.1c. Airtel imeongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya dakika za ndani ya mtandao (38.8%) na nje ya mtandao (30.5%).

#### Chati 1.3.1.1b Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti ndani ya mtandao kwa kila mtoa huduma



#### Chati 1.3.1.1c Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti nje ya mtandao kwa kila mtoa huduma



### 1.3.1.2 Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa miaka mitano iliyopita

Idadi ya dakika ndani na nje ya mtandao nchini katika kipindi cha miaka mitano iliyopita imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa 9% na 61%, mtawalia, kwa kila mwaka kuanzia 2019 hadi 2023. Idadi ya dakika nchini inaoneshwa katika Jedwali 1.3.1.2.


**Jedwali 1.3.1.2 Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa miaka mitano iliyopita**

	2019	2020	2021	2022	2023
Ndani ya mtandao	55,812,036,633	54,561,254,851	51,673,651,476	62,678,814,642	77,770,241,513
Nje ya mtandao	11,570,993,820	27,084,539,242	43,194,917,029	60,064,367,493	67,100,445,506
Jumla	67,383,030,453	81,645,794,093	94,868,568,505	122,743,182,135	144,870,687,019

Jedwali 1.3.1.2 linaonesha kuwa idadi ya dakika ndani ya mtandao ni kubwa ikilinganishwa na idadi ya dakika nje ya mtandao nchini. Hata hivyo, tofauti ya dakika hizo imeendelea kupungua kutokana na watoa huduma kutumia karibu viwango sawa vya bei za kupiga simu.

### 1.3.2 Idadi ya dakika za huduma ya sauti nje ya nchi

Idadi ya dakika kwenda na kutoka nje ya nchi imeoneshwa hapo chini.



Kielelezo kinaonesha kupungua kwa idadi ya dakika kwenda na kutoka nje ya nchi katika robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024. Idadi ya dakika kwenda nje ya nchi imeongezeka kwa 37.2%. Kwa upande mwingine, dakika kutoka nje ya nchi imeongezeka kwa 0.2%. Vilevile, takwimu zinaonesha kulikuwa na idadi kubwa ya dakika kwenda nje ya nchi ikilinganishwa na zilizotoka nje ya nchi.

Jumla ya dakika kwenda na kutoka Afrika Mashariki (EA) na nchi nyingine za kimataifa (RoW) kwa robo ya mwaka iliyoishia Sepetemba 2024 imeoneshwa katika Jedwali 1.3.2.

### Jedwali 1.3.2 Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA na RoW


	Kwenda EA	Kwenda RoW	Kutoka EA	Kutoka RoW
Julai	24,922,006	3,427,592	9,005,411	1,962,754
Agosti	37,936,673	3,527,043	9,058,028	2,012,347
Septemba	38,330,088	3,946,229	8,731,400	2,057,038
Jumla	101,188,767	10,900,864	26,794,839	6,032,139

Jedwali 1.3.2 linaonesha kulikuwa na dakika nyingi zaidi kwenda na kutoka EA katika mwezi Septemba 2024. Aidha, kulikuwa na dakika nyingi zaidi kwenda na kutoka RoW katika mwezi Septemba 2024 ikilinganishwa na miezi mingine ya robo iliyoishia Septemba 2024.

#### 1.3.2.1 Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA

Mgawanyo wa dakika kwenda na kutoka EA umeoneshwa kwenye Chati 1.3.2.1.

##### Chati 1.3.2.1 Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA




Chati 1.3.2.1 inaonesha kuwa dakika kwenda EA ni karibia mara 3 ya dakika kutoka EA.

#### 1.3.2.2 Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka RoW

Mgawanyo wa dakika kwenda na kutoka RoW umeoneshwa kwenye Chati 1.3.2.2.

##### Chati 1.3.2.2 Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka RoW



Chati 1.3.2.2 inaonesha kuwa dakika kwenda RoW ni karibia mara 2 ya dakika kutoka RoW.

### 1.3.2.3 Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA na RoW kwa miaka mitano iliyopita

Mwenendo wa idadi ya dakika kwenda na kutoka EA na RoW umeoneshwa katika Jedwali 1.3.2.3.

#### Jedwali 1.3.2.3 Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA na RoW kwa miaka mitano iliyopita

	2019	2020	2021	2022	2023
Kwenda EA	14,252,483	9,738,521	9,097,165	8,927,113	95,473,684
Kutoka EA	21,989,062	15,406,649	15,853,362	13,594,473	34,994,641
Kwenda RoW	43,297,997	38,014,133	24,856,947	26,034,131	19,510,999
Kutoka RoW	45,100,536	45,172,263	49,885,142	33,374,619	23,681,940

Kama inavyooneshwa katika Jedwali 1.3.2.3, idadi kubwa ya dakika zinakuja kutoka EA na RoW kuliko kwenda katika maeneo hayo isipokuwa katika mwaka 2023. Aidha, dakika za kwenda na kutoka EA na RoW zimekuwa zikipungua, isipokuwa mwaka 2023.

## 1.4 Idadi ya ujumbe mfupi wa maneno (SMS)

### 1.4.1 Idadi ya SMS ndani ya nchi

Robo mwaka inayoishia Juni 2024

**Bilioni 50.8**

Robo mwaka inayoishia Septemba  
2024

**Bilioni 47.6**

Badiliko  
**-6%** ↓

	SMS ndani ya mtandao	SMS nje ya mtandao	Jumla
Aprili - Juni 2024	Bilioni 21.5	Bilioni 29.3	Bilioni 50.8
Julai - Septemba 2024	Bilioni 20.2	Bilioni 27.4	Bilioni 47.6
<b>Badiliko</b>	<b>-6%</b>	<b>-7%</b>	<b>-6%</b>

Kielelezo kinaonesha kupungua kwa idadi ya SMS katika robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024 kwa 6% kwa SMS zinazotumwa ndani ya mtandao na kupungua kwa 7% kwa SMS zinazotumwa kutoka mtandao mmoja kwenda mitandao mingine. Kwa ujumla, idadi ya SMS imepungua kwa 6%. Idadi ya SMS kwa robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024 imeainishwa kwenye Jedwali 1.4.1.

#### Jedwali 1.4.1 Idadi ya SMS ndani ya nchi


	Julai	Agosti	Septemba	Jumla
Ndani ya mtandao	6,895,050,369	6,574,187,597	6,753,568,865	20,222,806,831
Nje ya mtandao	9,422,353,981	8,867,820,554	9,084,678,095	27,374,852,630
<b>Jumla</b>	<b>16,317,404,350</b>	<b>15,442,008,151</b>	<b>15,838,246,960</b>	<b>47,597,659,461</b>

Jedwali 1.4.1 linaonesha mabadiliko ya idadi ya SMS ndani na nje ya mtandao katika kipindi husika. Mwezi Julai 2024 ulikuwa na idadi kubwa ya SMS ikilinganishwa na mwezi Agosti na Septemba.

Kwa kipindi chote, mgawanyo wa SMS nje ya mtandao ulikuwa mkubwa (57.5%) kuliko ndani ya mtandao (42.5%). Hii inaonesha kuwa katika kipindi husika, hapakuwa na utofauti mkubwa wa bei za SMS ndani na nje ya mtandao. Mgawanyo wa SMS ndani na nje ya mtandao imeoneshwa kwenye Chati 1.4.1.



### Chati 1.4.1 Mgawanyo wa SMS ndani na nje ya mtandao



### 1.4.2 Idadi ya SMS za ndani ya nchi kwa miaka mitano iliyopita

Idadi ya SMS za ndani ya nchi kwa miaka mitano iliyopita imeoneshwa kwenye Jedwali 1.4.2.

**Jedwali 1.4.2 Idadi ya SMS za ndani ya nchi kwa miaka mitano iliyopita**

	2019	2020	2021	2022	2023
Ndani ya mtandao	53,787,444,093	61,971,569,487	58,875,779,663	65,358,270,089	84,818,793,761
Nje ya mtandao	51,650,529,287	71,072,186,913	78,200,512,436	88,154,239,625	121,727,776,013
<b>Jumla</b>	<b>105,437,973,380</b>	<b>133,043,756,400</b>	<b>137,076,292,099</b>	<b>153,512,509,714</b>	<b>206,546,569,774</b>

### 1.4.3 Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA na RoW


Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA na RoW imeoneshwa kwenye Jedwali 1.4.3.

**Jedwali 1.4.3 Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA na RoW**


	Kwenda	Kwenda RoW	Kutoka EA	Kutoka RoW
Julai	144,770	459,226	2,906,066	496,549,532
Agosti	163,135	452,329	3,790,707	548,094,184
Septemba	144,069	478,780	2,330,727	483,726,932
<b>Jumla</b>	<b>451,974</b>	<b>1,390,335</b>	<b>9,027,500</b>	<b>1,528,370,648</b>

Jedwali 1.4.3 linaonesha kuwa idadi kubwa ya SMS zilipokelewa kutoka EA na RoW kuliko zilizotumwa EA na RoW. Aidha, idadi kubwa zaidi ya SMS zilitumwa kwenda EA na RoW katika kipindi cha mwezi Agosti 2024, ikilinganishwa na miezi mingine katika kipindi husika. Uwiano wa SMS zilizotumwa na kupokelewa umeoneshwa kwenye Chati 1.4.3a na 1.4.3b.

**Chati 1.4.3a Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka EA**



**Chati 1.4.3b Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka RoW**



**1.4.4 Idadi ya SMS kwenda na kutoka EA na RoW kwa miaka mitano iliyopita**

Idadi ya SMS kwenda na kutoka EA na RoW kwa miaka mitano iliyopita imeoneshwa kwenye Jedwali 1.4.4.

**Jedwali 1.4.4 Idadi ya SMS kwenda na kutoka EA na RoW kwa miaka mitano iliyopita**

	2019	2020	2021	2022	2023
Kwenda EA	3,850,602	1,235,692	1,425,624	1,700,525	2,233,288
Kutoka EA	48,376,608	50,880,982	89,717,530	58,344,672	37,592,410
Kwenda RoW	6,834,308	2,718,443	3,191,041	3,574,956	5,448,764
Kutoka RoW	3,201,524,787	3,935,379,714	4,599,468,894	4,664,200,079	5,562,047,440

**1.5 Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu**

Vifaa vya masiliano vinavyotumia laini ya simu ndiyo kichocheo kikubwa katika kukuza matumizi ya huduma za mawasiliano ya simu/TEHAMA nchini. Idadi ya vifaa vilivyounganishwa kwenye mitandao ya simu imeoneshwa kwenye Jedwali 1.5.

## Jedwali 1.5 Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu

Aina ya kifaa	Idadi ya Vifaa	Ueneaji (Penetration)
Simu za rununu (Feature phones)	55,200,552	84.83%
Simu janja (Smartphones)	22,029,561	33.85%
Handheld	1,587,843	2.44%
Modem	650,138	1.00%
Portable (including Personal Digital Assistant PDA)	58,778	0.09%
Tablet	437,892	0.67%
Module	52,897	0.08%
WLAN Router	174,072	0.27%
Dongle	100,421	0.15%
Internet of Things (IoT) Devices	136,418	0.21%
Vehicle	12,655	0.02%
Computer	12,018	0.02%
Wearable	9,300	0.01%
Device for the Automatic Processing of Data (APD)	3,251	0.00%

Kufikia Septemba 2024, asilimia ya simu janja (smartphones) kwa idadi ya watu imeongezeka hadi 33.85% kutoka 31.55% iliyorekodiwa mwezi Juni 2024. Aidha, asilimia ya simu za rununu (feature phones) imeongezeka kutoka 82.6% na kufikia 84.83%. Ueneaji wa vifaa vingine vya mawasiliano miongoni mwa watu ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.5.

## 1.6 Idadi ya minara ya mawasiliano ya simu

Jedwali 1.6 linaonesha idadi ya minara ya mawasiliano ya simu katika mikoa mbalimbali ya Tanzania hadi Septemba 2024.

### Jedwali 1.6 Idadi ya Minara ya mawasiliano ya simu kwa kila mkoa

Mkoa	Idadi ya Minara ya Mawasiliano ya Simu
<b>Tanzania Bara</b>	
Arusha	409
Manyara	205
Kilimanjaro	334
Ruvuma	316
Dar es Salaam	1156
Pwani	303
Dodoma	415
Njombe	176
Tanga	395
Morogoro	421
Tabora	329
Mwanza	423
Geita	202
Kagera	355
Mara	273
Shinyanga	262
Iringa	274
Mbeya	379
Songwe	108
Katavi	94
Rukwa	205
Simiyu	144
Singida	211
Kigoma	287
Lindi	223
Mtwara	287
<b>Zanzibar</b>	
Mjini Magharibi	227
Kusini Pemba	53
Kaskazini Pemba	55
Kaskazini Unguja	25
Kusini Unguja	37
<b>Jumla</b>	<b>8,583</b>

Hadi kufikia Septemba 2024 kulikuwa na jumla ya minara 8,583, Dar es Salaam ikiongoza kwa kuwa na minara 1156, ikifuatiwa na Mwanza yenye minara 423. Mikoa yenye idadi ndogo zaidi ya minara kwa Tanzania Bara ni Katavi (94) na Songwe (108). Kwa upande wa Tanzania Visiwani, Mkoa wa Mjini Magharibi una idadi kubwa zaidi ya minara (227), huku mkoa wa Kaskazini Unguja ukiwa na idadi ndogo zaidi ya minara (25).

## 1.7 Idadi ya mitambo ya kurushia mawimbi ya simu

Jedwali 1.7 linaonesha idadi ya mitambo ya 2G, 3G, 4G na 5G kimkoa hadi kufikia Septemba 2024 .

### Jedwali 1.7 Idadi ya mitambo ya kurushia mawimbi ya simu kwa kila mkoa

Mkoa	Idadi ya mitambo ya kurushia mawimbi			
	BTS (2G)	NodeB (3G)	eNB (4G)	gNB (5G)
<b>Tanzania Bara</b>				
Arusha	669	643	629	29
Dar-es-salaam	2272	2441	2414	570
Dodoma	649	575	575	43
Geita	376	353	328	6
Iringa	374	320	313	4
Kagera	489	446	406	1
Katavi	156	133	132	1
Kigoma	467	409	384	3
Kilimanjaro	528	510	498	7
Lindi	333	251	266	1
Manyara	324	266	270	1
Mara	396	358	347	4
Mbeya	552	531	522	16
Morogoro	647	587	574	9
Mtwara	403	336	325	1
Mwanza	723	694	674	25
Njombe	297	255	252	3
Pwani	451	419	415	11
Rukwa	274	229	214	1
Ruvuma	423	329	331	2
Shinyanga	351	336	299	6
Simiyu	268	228	205	2
Singida	322	288	274	3
Songwe	233	198	191	13
Tabora	509	449	397	4
Tanga	604	534	524	3
<b>Zanzibar</b>				
Kaskazini Pemba	58	58	54	0
Kaskazini Unguja	74	76	75	4
Kusini Pemba	63	63	58	1
Kusini Unguja	113	114	113	4
Mjini Magharibii	181	208	201	55
<b>Jumla</b>	<b>13,579</b>	<b>12,637</b>	<b>12,260</b>	<b>834</b>


Jedwali 1.7 linaonesha kuenea kwa kiasi kikubwa kwa teknolojia ya 2G na 3G, ikiwa na BTS 13,579 na NodeB 12,637. Japokuwa teknolojia ya 4G haijaenea kama 2G na 3G, idadi ya eNB za 4G zimefika 12,260. Aidha, gNB za 5G zimeongezeka kwa kiasi cha asilimia 6 zikiwa zimefika 834, ikiwa zimeenea zaidi katika maeneo ya mijini kama vile Dar es Salaam na Mjini Magharibi. Hata hivyo, Dar es Salaam inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya mitambo ya kurushia mawimbi ya mawasiliano kwa teknolojia zote (2G, 3G, 4G na 5G), na kuifanya kuwa kitovu cha mawasiliano nchini.

# 2. Takwimu za Pesa Mtandao

Sehemu hii inawasilisha takwimu za huduma za pesa mtandao zinazotolewa na watoa huduma za pesa mitandao (Mobile Money Operators) kulingana na idadi ya akaunti za pesa mtandao na miamala.

## 2.1 Akaunti za pesa mtandao

Idadi ya akaunti za pesa mtandao ambazo zilitumika angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita iliongezeka kutoka akaunti milioni 55.7 katika robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024 hadi milioni 60.8 katika robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024.




Jedwali 2.1 Idadi ya akaunti za pesa mtandao

	JULAI	AGOSTI	SEPTEMBERA
Airtel Money	11,197,981	11,319,425	11,435,679
Azam Pesa	631,364	829,041	891,751
Halo Pesa	4,781,535	4,915,390	5,096,559
M-Pesa	21,387,479	21,811,045	22,445,464
Tigo Pesa	18,707,319	18,514,018	19,492,440
T-Pesa	1,434,579	1,445,981	1,453,640
<b>Jumla</b>	<b>58,140,257</b>	<b>58,834,900</b>	<b>60,815,533</b>

Jedwali 2.1 linaonesha kuwa akaunti za pesa mtandao ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 2.3 kwa mwezi katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2024. Mgawanyo wa akaunti za pesa mtandao umeoneshwa kwenye Chati 2.1.

Chati 2.1 Mgawanyo wa akaunti za pesa mtandao



Chati 2.1 inaonesha kuwa soko la pesa mtandao lina ushindani, huku M-pesa ikiongoza kwa kuwa na asilimia 36.9.

## 2.2 Idadi ya miamala ya pesa mtandao

Idadi ya miamala ya pesa mtandao kwa akaunti zilizoweka na kutuma pesa kwa njia ya pesa mtandao katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita ya robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024 imeoneshwa kwenye Jedwali 2.2a.

### Jedwali 2.2a Idadi ya miamala ya pesa mtandao

	Julai	Agosti	Septemba
Airtel Money	87,014,790	89,257,370	92,666,780
Azam Pesa	1,867,674	1,807,564	5,052,925
Halo Pesa	30,675,639	33,192,501	35,044,286
T- Pesa	658,305	500,960	502,976
Tigo Pesa	83,656,081	86,972,073	87,929,210
M-Pesa	79,089,897	73,786,751	89,685,384
<b>Jumla</b>	<b>282,962,386</b>	<b>285,517,219</b>	<b>310,881,561</b>

Jedwali 2.2b linaonesha idadi ya miamala ya pesa mtandao kwa miaka mitano iliyopita. Miamala ya pesa mtandao iliongezeka kutoka bilioni 3 mwaka 2019 hadi bilioni 5.3 kwa mwaka 2023, sawa na 19% ya ukuaji kwa kila mwaka. Katika kipindi hicho, wastani wa miamala kwa kila mteja ulipungua kutoka miamala 117 mwaka 2019 hadi 100 mwaka 2023.

### Jedwali 2.2b Idadi ya usajili na miamala ya pesa mtandao kwa miaka mitano iliyopita

Mwaka	Idadi ya akaunti	Idadi ya miamala	Wastani
2019	25,864,318	3,021,142,958	117
2020	32,268,630	3,412,210,062	106
2021	35,285,767	3,752,084,894	106
2022	40,953,496	4,195,899,414	102
2023	52,875,129	5,273,086,154	100



# 3. Takwimu za huduma ya Intaneti

## 3.1 Laini za Intaneti

Idadi ya laini za Intaneti inatokana na laini ambazo zimetumia huduma ya Intaneti angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita, bila kujali teknolojia iliyotumika (FTTX, 2G - GPRS na EDGE, 3G, 4G, au 5G).

Idadi ya laini za Intaneti imeongezeka kwa 5% kutoka milioni 39.3 kwa robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024 hadi milioni 41.4 kwa robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024.

Kufikia Juni 2024

**Milioni 39.3**

Kufikia Septemba 2024

**Milioni 41.4**



**5%**

Idadi ya laini za Intaneti kwa robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024 imeoneshwa kwenye Jedwali 3.1a

### Jedwali 3.1a Idadi ya laini za Intaneti kufikia mwisho wa kila mwezi katika robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024

Mwezi	Mobile Wireless	Fixed Wireless	Fixed Wired	Jumla
Julai	40,238,289	49,905	67,485	40,355,679
Agosti	40,614,846	52,893	68,684	40,736,423
Septemba	41,246,748	59,605	70,192	41,376,545

### Jedwali 3.1b Idadi ya laini za Intaneti kwa teknolojia kufikia Septemba 2024


Teknolojia	Julai	Agosti	Septemba
2G	18,112,328	18,306,340	18,340,688
Intaneti ya kasi kwa huduma ya simu	22,125,961	22,308,506	22,906,060
Faiba Nyumbani (FTTH)	58,030	59,656	59,743
Faiba Ofisini (FTTO)	9,455	9,028	10,449
Intaneti ya kasi kwa huduma ya simu (zingine)	49,905	52,893	59,605
<b>Jumla</b>	<b>40,355,679</b>	<b>40,736,423</b>	<b>41,376,545</b>

Jedwali 3.1b linaonesha kuwa Intaneti ya kasi kwa huduma ya simu ndiyo njia inayopendelewa zaidi kupata Intaneti, ikiwa na laini 22,906,060. Teknolojia ya 2G bado ina matumizi makubwa, ikiwa na laini 18,340,688. Teknolojia za Faiba Nyumbani (Fiber to the Home - FTTH) na Faiba Ofisini (Fiber to the Office - FTTO) zina idadi ndogo ya laini 59,743 na 10,449 mtawalia.

### Jedwali 3.1c Idadi ya laini za Intaneti kwa njia ya simu kwa kila mtoa huduma kufikia Septemba 2024


Mtoa Huduma	Mobile Subscriptions
TTCL	1,514,264
Tigo	13,391,905
Halotel	4,470,738
Airtel	10,363,269
Vodacom	11,506,572
<b>Jumla</b>	<b>41,246,748</b>

### Chati 3.1a Mgawanyo wa laini za Intaneti kwa njia ya simu kwa kila mtoa huduma




■ TTCL ■ Tigo ■ Halotel ■ Airtel ■ Vodacom

### Chati 3.1b idadi ya laini za Intaneti (fixed) kwa kila mtoa huduma



Idadi ya laini za Intaneti kwa miaka mitano iliyopita imeoneshwa kwenye Chati 3.1c


### Chati 3.1c Idadi ya laini zinazotumia huduma ya Intaneti kwa miaka mitano iliyopita



Chati 3.1c inaonesha wastani wa ongezeko la kila mwaka la 9.8% la idadi ya laini zinazotumia huduma ya Intaneti kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Laini zinazotumia Intaneti ziliongezeka kutoka milioni 25.8 mwaka 2019 hadi milioni 35.9 mwaka 2023.

### 3.2 Matumizi ya huduma ya Intaneti kwa mwezi

Matumizi ya mwezi ya huduma ya Intaneti huhesabiwa kama kiasi cha data (katika Petabytes) kilichotumiwa katika kipindi hicho. (Kumbuka kuwa 1 Petabyte = 1000<sup>3</sup> Megabytes).



### Jedwali 3.2 Kiasi cha data kilichotumika katika robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024

	Julai	Agosti	Septemba
Kiasi cha data (MB)	187,513,225,054	195,058,997,727	200,886,387,461
Usajili	40,355,679	40,736,423	41,376,545
MB kwa kila usajili	4,647	4,788	4,855

Jedwali 3.2 linaonesha kuwa kila mteja alitumia wastani wa MB 4,855 kwa mwezi Septemba.

### 3.3 Uwezo wa kuunganishi cha Intaneti kimataifa

Uwezo wa kuunganisha huduma ya Intaneti kwenda nje na kuja ndani ya nchi (International Internet link capacity) unasaidia matumizi ya Intaneti ndani na nje ya nchi. Jedwali 3.3 linaonesha kuwa nchi ina uwezo wa 15,332 Gbps kwa ajili ya uunganishaji wa huduma ya Intaneti.

### Jedwali 3.3 Uwezo wa kuunganisha huduma ya Intaneti

	Uwezo unaotoka (Gbps)	Uwezo unaoingia (Gbps)
Jumla ya uwezo unaomilikiwa	17,200	17,200
Uwezo unaotumika (activated)	1,868	1,868
Uwezo unaopatikana kwa uwezeshaji mpya	15,332	15,332

### 3.4 Usimikaji na kasi ya Intaneti

Uwekezaji katika miundombinu ya mawasiliano umeongeza kasi na usambaaji wa Intaneti ya kasi (broadband), kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 3.4.

#### Jedwali 3.4 Usambaaji na kasi ya huduma ya Intaneti kufikia Septemba 2024

Kiashiria	Aina	Juni 2024	Septemba 2024
Asilimia ya watu waliofikiwa na Intaneti ya kasi (3G, 4G au zaidi)	3G	89%	90%
	4G	83%	85%
	5G	15%	18%
Asilimia ya eneo lilofikiwa na Intaneti ya kasi (3G, 4G au zaidi)	3G	73%	74%
	4G	69%	70%
	5G	2%	2.2%

Jedwali 3.4, linaonesha kupanuka kwa wigo wa 3G, 4G na 5G kufikia 90%, 85%, na 18% ya watu nchini, mtawalia. Aidha, asilimia ya eneo lilofikiwa na Intaneti ya kasi ya 3G, 4G na 5G ni 74%, 70%, na 2.2%, mtawalia.

#### Kiashiria cha Ubora wa huduma ya Intaneti: Wastani wa kasi ya kupakua na kupakia (katika Mbit/s)

	↓ Kupakua Mbps	↑ Kupakia Mbps	⇄ Latency ms
Mobile Broadband	13.2	11.3	47.4
Fixed Broadband	40.9	34.6	22.1

### 3.5 Idadi ya viko vya Intaneti

Jumla ya idadi ya viko vilivyosajiliwa iliongezeka kutoka 30,698 mwishoni mwa Juni 2024 hadi 31,584 mwishoni mwa Septemba 2024, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 3.5.

#### Jedwali 3.5 Idadi ya viko vya Intaneti

Kikoa	Juni 2024	Septemba 2024
co.tz	24,085	24,796
or.tz	2,652	2,696
ac.tz	1,146	1,160
go.tz	902	913
.tz	1,614	1,706
sc.tz	244	256
ne.tz	31	33
me.tz	8	9
info.tz	2	2
hotel.tz	3	2
Mobi.tz	5	5
tv.tz	3	2
mil.tz	3	4
Jumla	30,698	31,584

## 4. Takwimu za Huduma za Utangazaji

Sehemu hii inawasilisha takwimu za huduma za televisheni kwa njia ya mitambo iliyosimikwa ardhini (DTT), setilaiti (DTH), na kwa njia ya waya (Cable TV).

### 4.1 Visimbuzi vilivyolipiwa


Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita ili kupata huduma za utangazaji za televisheni imeoneshwa kwenye Jedwali 4.1. Jedwali linaonesha kuwa Azam Media Limited ina idadi kubwa ya visimbuzi vya DTT vilivyolipiwa vifurushi ikilinganishwa na watoa huduma wengine, ikifuatiwa na Star Media Limited mtawalia. Aidha, Azam Media Limited ina idadi kubwa ya visimbuzi vya DTH vilivyolipiwa ikilinganishwa na watoa huduma wengine, ikifuatiwa na Star Media Limited. Kwa ujumla idadi ya visimbuzi vya DTH vilivyolipiwa vifurushi ni vingi kuliko visimbuzi vya DTT.

#### Jedwali 4.1 Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa kwa kila mtoa huduma

Mtoa huduma	Visimbuzi vya DTT	Visimbuzi vya DTH	Jumla ya visimbuzi vilivyolipiwa
Azam Media Limited	271,962	1,084,702	1,356,664
Agape Associates	1,840		1,840
Star Media Limited	230,000	247,236	477,236
Zuku	-	21,687	21,687
Basic Transmissions Limited (Continental)	37,659	31,309	68,968
Multichoice Tanzania Limited (DSTv)	-	234,415	234,415
Basic Transmissions Limited (Digitek)	15,000	-	15,000
<b>Jumla</b>	<b>556,461</b>	<b>1,619,349</b>	<b>2,175,810</b>

Ramani 4.1 inaonesha idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa vifurushi kwa kila mkoa. Dar es Salaam imeshika nafasi ya kwanza (713,630), Mwanza ya pili (178,381), Mbeya ya tatu (156,664), Arusha ni ya nne (133,746) na mikoa mingine ni kama ilivyooneshwa kwenye ramani.


**Ramani 4.1 Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa vifurushi kwa kila mkoa**



**4.2 Idadi ya visimbuzi vilivyouzwa kwa miaka mitano iliyopita**

Idadi ya visimbuzi vya DTT na DTH vilivyouzwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita imeoneshwa kwenye Chati 4.2.

**Chati 4.2 Idadi ya visimbuzi vilivyouzwa kwa miaka mitano iliyopita**



Kuna ongezeko la visimbuzi vya DTT na DTH kama ilivyooneshwa kwenye Chati 4.2, ambapo hadi mwaka 2023 kulikuwa na idadi kubwa ya visimbuzi vilivyouzwa.


### 4.3 Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya

Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya (Cable TV subscriptions) zimeongezeka kwa 2% kutoka 18,820 kwa robo mwaka inayoishia Juni 2024 na kufikia 19,153 katika kipindi cha robo mwaka inayoishia Septemba 2024.



Idadi ya televisheni kwa kila mkoa katika kipindi husika umeoneshwa kwenye Chati 4.3.

### Chati 4.3 Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kufikia Septemba 2024





Kwa mikoa yote Tanzania Bara, Shinyanga inaongoza kwa kuwa na televisheni nyingi zinazopokea maudhui kwa njia ya waya (4,845), ikifuatiwa na Tabora (2,118), na Mwanza (2,075). Aidha, mikoa yenye idadi ndogo ya televisheni zinazopokea maudhui kwa njia ya waya ni Tanga (230), ikifuatiwa na Manyara (91) na ya mwisho ni Mbeya (64).

#### 4.4 Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa miaka mitano iliyopita

Idadi ya televisheni zinazopokea maudhui kwa njia ya waya iliongezeka kati ya 2020 na 2022. Aidha, idadi hiyo ilipungua mwaka 2023 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 4.4. Kupungua kwa idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa mwaka 2023 kumechangiwa na kuongezeka kwa usambaaji wa televisheni kwa njia ya DTT na DTH.

##### Jedwali 4.4 Idadi ya televisheni kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita

	2019	2020	2021	2022	2023
Usajili	15,245	14,350	19,739	22,295	16,223

#### 4.5 Ueneaji wa huduma za utangazaji

Takwimu zinaonesha kuna utofauti wa ueneaji wa huduma za utangazaji kwa njia ya DTT, DTH na redio kama inavyoonekana kwenye Jedwali 4.5.

##### Jedwali 4.5 Ueneaji wa huduma za utangazaji kwa kipindi cha Septemba 2024

Kiashiria	Septemba 2024
% ya watu waliofikiwa na DTT	58%
% ya watu waliofikiwa na DTH	100%
% ya watu waliofikiwa na redio za FM	78%
% ya eneo lililofikiwa na DTT	33%
% ya eneo lililofikiwa na DTH	100%
% ya eneo lililofikiwa na redio za FM	56.5%

## 5. Takwimu za Huduma ya Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto (Courier)

Sehemu hii inawasilisha takwimu za huduma ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto, zilizotumwa na kupokelewa, kwenda na kutoka ndani ya nchi, Afrika Mashariki (EA) na mataifa mengine (RoW).

### 5.1 Idadi ya masanduku ya posta

Shirika la Posta Tanzania (TPC) linatoa huduma za msingi za posta za masanduku na mifuko binafsi ya barua kwa watu binafsi na kampuni. Idadi ya masanduku na mifuko binafsi katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2024, ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 5.1.

#### Jedwali 5.1 Masanduku na mifuko binafsi ya barua

Mwezi	Masanduku ya barua	Mifuko binafsi ya barua	Jumla
Julai	158,006	67	<b>158,073</b>
Agosti	158,006	67	<b>158,073</b>
Septemba	158,006	67	<b>158,073</b>

### 5.2 Wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Idadi ya wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto kwa kipindi husika imeoneshwa kwenye Jedwali 5.2.

#### Jedwali 5.2 Idadi ya wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi/vipeto

Mwezi	Kampuni/Taasisi	Wateja binafsi	Jumla
Julai	1,168	35,628	<b>36,796</b>
Agosti	1,801	70,316	<b>72,117</b>
Septemba	708	47,215	<b>47,923</b>

### 5.3 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi imepungua kwa 10% kutoka 552,165 kwa mwezi Aprili hadi Juni 2024 na kufikia 495,521 kwa mwezi Julai hadi Septemba 2024.


Takwimu zinaonesha nyaraka (documents) zilitumwa zaidi katika kipindi cha robo mwaka iliyoishia Septemba 2024, ikifuatiwa na Barua. Mizigo (Cargo) vimetumwa kwa idadi ndogo zaidi katika kipindi hicho. Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa katika kipindi husika zimeoneshwa kwenye Jedwali 5.3.

### Jedwali 5.3 Idadi ya bidhaa za kipošta zilizotumwa ndani ya nchi kwa robo mwaka iliyoishia Septemba 2024

Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Julai	55,999	64,289	5,391	55,592	114	181,385
Agosti	57,709	17,660	2,595	64,622	799	143,385
Septemba	52,882	63,729	4,805	49,201	134	170,751
<b>Jumla</b>	<b>166,590</b>	<b>145,678</b>	<b>12,791</b>	<b>169,415</b>	<b>1,047</b>	<b>495,521</b>

Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kipošta zilizotumwa na TPC na watoa huduma wengine wa huduma za usafirishaji ndani ya nchi umeoneshwa katika Chati 5.3. TPC ikiwa na idadi kubwa zaidi (61%) ya bidhaa za kipošta zilizotumwa ndani ya nchi ikilinganishwa na watoa huduma binafsi.

#### Chati 5.3 Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kipošta zilizotumwa ndani ya nchi



### 5.4 Idadi ya bidhaa za kipošta zilizotumwa nje ya nchi

Idadi ya bidhaa za kipošta zilizotumwa nje ya nchi kupitia TPC na watoa huduma wengine wa huduma ya usafirishaji katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2024 imeoneshwa kwenye jedwali 5.4a.

#### Jedwali 5.4a Idadi ya bidhaa za kipošta zilizotumwa nje ya nchi

	Apr - Jun 2024	Jul - Sept 2024
TPC	39,308	18,483
Watoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto	13,763	15,083
<b>Jumla</b>	<b>53,071</b>	<b>33,566</b>

Jedwali 5.4b linaonesha idadi ya bidhaa za kipošta zilizotumwa nje ya nchi. Takwimu zinaonesha kuwa barua zimetumwa zaidi nje ya nchi katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2024, ikifuatiwa na nyaraka.

#### Jedwali 5.4b Idadi ya bidhaa za kipošta zilizotumwa nje ya nchi

Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Julai	3,853	1,005	587	1,770	1,342	7,215
Agosti	4,516	5,653	171	4,657	931	14,997
Septemba	6,709	1,589	793	2,263	1,253	11,354
<b>Jumla</b>	<b>15,078</b>	<b>8,247</b>	<b>1,551</b>	<b>8,690</b>	<b>3,526</b>	<b>33,566</b>

## 5.5 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka ndani ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kupitia TPC na watoa huduma wengine wa usafirishaji wa vifurushi na vipeto ilikuwa 443,977.

### Jedwali 5.5 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa ndani ya nchi kwa robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024

Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Julai	38,428	74,202	5,081	31,849	90	149,650
Agosti	42,441	26,709	2,789	63,053	979	135,971
Septemba	53,304	58,167	3,066	43,812	7	158,356
<b>Jumla</b>	<b>134,173</b>	<b>159,078</b>	<b>10,936</b>	<b>138,714</b>	<b>1,076</b>	<b>443,977</b>

## 5.6 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi ni 60,712 kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2024 kama ilivyooneshwa kwenye jedwali 5.6a.

### Jedwali 5.6a Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi

	Apr - Jun	Jul - Sept
TPC	53,493	38,668
Watoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto	150,209	22,044
<b>Jumla</b>	<b>203,702</b>	<b>60,712</b>


Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi zimeoneshwa kwenye Jedwali 5.6b. Barua kutoka nje ya nchi zimepokelewa kwa idadi kubwa zaidi ikilinganisha na bidhaa nyingine katika robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024, wakati mizigo kutoka nje ya nchi ilipokelewa kwa idadi ndogo zaidi katika kipindi husika.

### Jedwali 5.6b Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi

Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Julai	6,637	4,673	2,449	4,125	97	17,981
Agosti	8,572	5,904	5,499	5,131	5	25,111
Septemba	9,717	2,022	3,972	1,910	-	17,620
<b>Jumla</b>	<b>24,926</b>	<b>12,599</b>	<b>11,920</b>	<b>11,166</b>	<b>102</b>	<b>60,712</b>

Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa na kupokelewa unaonesha kuwa Tanzania ilituma bidhaa za kiposta chache zaidi nje ya nchi (36%) kuliko ilivyopokea (64%) kama ilivyooneshwa kwenye Chati 5.6b.

### Chati 5.6 Mgawanyo wa bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi na kupokelewa kutoka nje ya nchi




■ Bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi  
 ■ Bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi

### 5.7 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani na nje ya nchi kwa miaka mitano iliyopita

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa kwa miaka mitano iliyopita imeoneshwa kwenye Chati 5.7.

#### Chati 5.7 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani na nje ya nchi kwa miaka mitano iliyopita




Chati 5.7 inaonesha kuwa bidhaa za kiposta nyingi zaidi zilitumwa ndani ya nchi kuliko nje ya nchi. Aidha, idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa kwa ujumla imekuwa ikishuka.

## 5.8 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi na kupokelewa kutoka nje ya nchi kwa miaka mitano iliyopita

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi imepungua kutoka bidhaa 2,873,312 kwa 2019 na kufikia 493,053 kwa 2023 kama inavyooneshwa kwenye Chati 5.8. Aidha, idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi ilipungua.

**Chati 5.8 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi na zilizopokelewa kutoka nje ya nchi kwa miaka mitano iliyopita**



# 6. Ubora wa Huduma, Ufuatiliaji wa Masharti ya Leseni na Majaribio ya Ulaghai Mtandaoni


## 6.1 Ubora wa huduma za simu na Intaneti

Vipimo vya ubora wa huduma (Quality of Service - QoS) wa huduma ya simu na Intaneti zinazotolewa na mitandao ya simu nchini vilifanyika kuanzia Julai hadi Septemba 2024 kwa kuzingatia vigezo vya QoS na mbinu za vipimo vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2018.

### 6.1.1 Upatikanaji wa mtandao

Upatikanaji wa mtandao ni kiashiria kinachoonesha upatikanaji wa mtandao wa simu wakati watumiaji wanataka kutumia huduma za mtandao huo. Lengo ni kufikia zaidi ya 99% (>99%).

Tigo ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika. Airtel na Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tatu kati ya maeneo kumi na nne, TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na mbili. Halotel zilifikia lengo kwenye maeneo kumi kati ya kumi na nne, kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.1.




Chati 6.1.1. Upatikanaji wa Mtandao (%) (Lengo ni zaidi ya 99%)

### 6.1.2 Simu zilizoshindwa kuunganishwa

Simu zilizoshindwa kuunganishwa hupimwa kwa asilimia ya simu ambazo hazikuweza kuunganishwa baada ya kupiga kwa sababu za kiufundi. Lengo ni chini ya 2%.

Tigo ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika. Airtel zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na mbili, Halotel na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na moja, na TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo sita kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.2.




Chati 6.1.2 Simu zilizoshindwa kuunganishwa

### 6.1.3 Simu zilizokatika

Simu zilizokatika hupimwa kwa asilimia ya simu zinazokatika kwa sababu za kiufundi kabla ya wahusika kumaliza mazungumzo yao na mmoja wao kukata simu (simu zilizokatwa). Lengo ni chini ya 2%.

Watoa huduma wote wa mawasiliano ya simu walifikisha lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika, kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.3.




Chati 6.1.3. Matokeo ya Simu zilizokatika

### 6.1.4 Upatikanaji wa huduma ya 2G

Upatikanaji wa huduma ya 2G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Wateja hawawezi kupata huduma za mtandao wa simu za 2G katika maeneo ambayo hayana mtandao au yenye mtandao duni. Lengo la juu kwa teknolojia ya 2G ni -85 dBm.



Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na mbili kati ya kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika. Airtel alifikia lengo kwenye maeneo nane kati ya maeneo tisa, Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo matano kati ya maeneo kumi, TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo matatu na kati ya matano yaliopimwa na Tigo ilifikia lengo kwenye eneo moja kati ya maeneo mawili kama inavyooneshwa Chati 6.1.4.




Chati 6.1.4. Matokeo linganishi kwenye upatikanaji wa huduma ya 2G

### 6.1.5 Upatikanaji wa huduma ya 3G

Upatikanaji wa huduma ya 3G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Wateja hawawezi kupata huduma za mtandao wa simu za 3G katika maeneo ambayo hayana mtandao au yenye mtandao duni. Lengo la juu kwa teknolojia ya 3G ni -85 dBm.

Halotel na Tigo ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika. Vodacom na Airtel zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tatu, na TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na mbili kati ya maeneo kumi na nne, kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.5.



Chati 6.1.5. Matokeo ya kulinganisha upatikanaji wa huduma ya 3G

### 6.1.6 Upatikanaji wa huduma ya 4G

Upatikanaji wa huduma ya 4G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Wateja hawawezi kupata huduma za mtandao wa simu za 4G katika maeneo ambayo hayana mtandao au yenye mtandao duni. Lengo la juu kwa teknolojia ya 4G ni -95 dBm.

Tigo na TTCL zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika. Vodacom na Airtel zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na mbili. Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na moja kati ya maeneo kumi na nne yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.6.





Chart 6.1.6. Matokeo linganishi kwenye upatikanaji wa huduma ya 4G

### 6.1.7 Simu zilizofanikiwa

Simu zilizofanikiwa hupimwa kwa asilimia ya simu zilizokamilishwa baada ya upigaji, kwamba hazikuzuiwa au kukatika. Lengo ni sawa na au zaidi ya 95% (=>95%).

Airtel, Tigo na Vodacom walifikisha lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ya huduma yaliyopimwa. Halotel alifikisha lengo kwenye maeneo kumi na tatu, TTCL alifikisha lengo kwenye maeneo tisa, kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.7.




Chati 6.1.7. Matokeo ya kulinganisha simu zilizofanikiwa

### 6.1.8 Simu kuhamishika

Simu kuhamishika hupimwa kwa jinsi simu za sauti zinavyohamishwa kutoka mnara mmoja wa mawasiliano hadi mwingine bila kukatika pale mtumiaji anapotoka eneo moja kwenda jingine. Lengo ni sawa na au zaidi ya 98% (=>98%).

Airtel, Halotel, Tigo na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika, na TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na mbili, kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.8.




Chati 6.1.8. Matokeo ya kulinganisha simu kuhamishika

### 6.1.9 Ubora wa Sauti

Ubora wa Sauti ni kipimo cha utambuzi wa ubora wa sauti wakati wa mazungumzo ya simu. Kiwango cha alama ya ubora wa sauti ni kati ya 1 hadi 5, huku 1 ikiwa duni na 5 ikiwa ni ubora mzuri wa sauti. Lengo ni wastani wa sampuli zote za vipimo vya ubora wa sauti kuwa zaidi ya 3.5.

Airtel, Tigo, TTCL na Vodacom zilifikisha lengo kwenye maeneo yote kumi na tatu ambapo vilipimo vilifanyika, Halotel ilifikisha lengo kwenye maeneo yote kumi ambapo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.9.




Chati 6.1.9. Matokeo ya kulinganisha kwenye Ubora wa Sauti

### 6.1.10 Kasi ya kupakua data

Kasi ya kupakua data ni kipimo cha kasi ya uhamishaji data kwenye mtandao. Hupimajinsi data inavyohamishwa haraka kutoka kwa itifaki (protocol) ya uhamishaji faili (File Transfer Protocol - FTP) hadi kwa kifaa cha mawasiliano ya simu. Lengo ni wastani kuwa sawa au zaidi ya 4000 Kbps.

Watoa huduma wote wa mawasiliano ya simu walifikisha lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika, kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.10.




Chati 6.1.10. Matokeo linganishi kwenye kasi ya kupakua data

### 6.1.11 Muda wa kupata huduma ya data

Muda wa kupata huduma ya data hupimwa kwa muda ambao kifaa cha mtumiaji huchukua kutuma ombi na kupokea jibu kutoka kwenye seva. Lengo ni wastani kuwa chini ya 400ms ( $\leq 400ms$ ).

Watoa huduma wote wa mawasiliano ya simu walifikisha lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika, kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.11.




Chati 6.1.11. Matokeo linganishi ya muda wa kupata huduma ya data

### 6.1.12 Simu kushindwa kusoma mtandao

Simu kushindwa kusoma mtandao hupimwa kwa asilimia ambayo simu ya mkononi inaposhindwa kuunganishwa kwenye mtandao ikiwa imewashwa. Lengo ni chini ya 2% (<2%).

Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika. Tigo na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na moja kati ya maeneo kumi na nne, Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo tisa, na TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo saba kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.12.



Chati 6.1.12. Matokeo ya kulinganisha simu kushindwa kusoma mtandao

### 6.1.13 Muda wa simu kusoma mtandao

Muda wa simu kusoma mtandao ni muda ambao simu ya mkononi inachukua kuunganishwa kwenye mtandao ikiwa imewashwa. Lengo ni chini ya sekunde 5 (<5s).

Watoa huduma wote wa mawasiliano ya simu walifikisha lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika, kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.13.




Chart 6.1.13. Matokeo ya kulinganisha muda wa simu kusoma mtandao.

### 6.1.14 Muda wa kuanzisha simu

Muda wa kuanzisha simu hupimwa kwa muda ambao simu inachukua kuunganishwa baada ya kupiga. Lengo ni chini ya sekunde 10 (<10s).

Watoa huduma wote wa mawasiliano ya simu walifikisha lengo kwenye maeneo yote kumi na nne ambapo vipimo vilifanyika, kama inavyooneshwa kwenye Chati 6.1.14.




Chart 6.1.14. Matokeo ya kulinganisha muda wa kuanzisha simu

Matokeo ya upimaji wa ubora wa huduma za simu na Intaneti kwa kipindi cha Juni hadi Septemba 2024 yanaonesha kuwa Airtel ilikuwa na 97%, Vodacom 93%, Tigo 98%, Halotel 90%, na TTCL 86%, kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 6.1.

### Jedwali 6.1 Matokeo ya ubora wa huduma za simu na Intaneti kwa robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024 na Septemba 2024

Mtoa huduma	Juni 2024	Septemba 2024	Badiliko
Tigo	99%	98%	-1%
Airtel	98%	97%	-1%
Vodacom	96%	93%	-3%
Halotel	93%	90%	-3%
TTCL	78%	86%	10%
<b>Wastani wa Sekta</b>	<b>91%</b>	<b>93%</b>	<b>0.16%</b>

Kwa kulinganisha vipindi hivyo, Jedwali 6.1 linaonesha kuwa watoa huduma wanne wameboresha huduma zao katika robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024 huku ubora wa huduma ukishuka kwa mtoa huduma mmoja. Aidha, wastani wa ubora wa huduma za simu na Intaneti kwenye sekta umepanda kwa 0.16%.

## 6.2 Utekelezaji wa masharti ya leseni ya utangazaji

Ufuatiliaji wa maudhui kwa watoa huduma za utangazaji wa kitaifa nchini vilifanyika kuanzia Julai hadi Septemba 2024 kwa kuzingatia vigezo vya QoS na mbinu za vipimo vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2018.

### 6.2.1 Uwasilishaji na uzingatiaji wa ratiba ya vipindi

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kuwasilisha ratiba (muda, mpangilio, na idadi) na kuzingatia ratiba ya vipindi wanavyokusudia kurusha hewani. Uzingatiaji wa uwasilishaji wa mpangilio wa vipindi na kufuata ratiba kwa robo mwaka iliyotathminiwa umeonyeshwa kwenye Jedwali 6.2.1a na 6.2.1b hapa chini.

#### Jedwali 6.2.1a Uwasilishaji na uzingatiaji wa mpango wa vipindi vya televisheni

TV	Uwasilishaji wa ratiba ya vipindi	Uzingatiaji wa ratiba ya vipindi
ITV	Imekidhi	Imekidhi
UTV	Imekidhi	Imekidhi
Tumaini TV	Imekidhi	Haijakidhi
Channel Ten	Haijakidhi	Haijakidhi
East Africa TV	Imekidhi	Imekidhi
Star TV Tanzania	Imekidhi	Haijakidhi
TBC 1	Imekidhi	Imekidhi
TV Imaan	Imekidhi	Imekidhi
Arise and Shine	Imekidhi	Haijakidhi
WRM TV	Imekidhi	Imekidhi
Clouds TV	Haijakidhi	Haijakidhi
Hope Channel Tanzania	Imekidhi	Haijakidhi
Upendo TV	Imekidhi	Haijakidhi
Mahaasin TV	Imekidhi	Haijakidhi
Channel Ten Plus	Haijakidhi	Haijakidhi
TVE	Haijakidhi	Haijakidhi

#### Jedwali 6.2.1b Uwasilishaji na uzingatiaji wa mpango wa vipindi vya redio

Redio	Uwasilishaji wa ratiba ya vipindi	Uzingatiaji wa ratiba ya vipindi
Radio One	Haijakidhi	Haijakidhi
TBC Taifa	Imekidhi	Imekidhi
Adventist World Radio (AWR)	Imekidhi	Haijakidhi
Clouds FM	Imekidhi	Imekidhi
East Africa Radio	Imekidhi	Imekidhi
EFM	Imekidhi	Imekidhi
Wasafi FM	Imekidhi	Imekidhi
TBC International	Imekidhi	Imekidhi
Radio Free Africa	Haijakidhi	Haijakidhi
Bongo FM	Haijakidhi	Haijakidhi
Radio Maria	Haijakidhi	Haijakidhi

## 6.2.2 Utofauti wa vipindi, maudhui ya elimu na uzingatiaji wa dakika tisini ya utoaji wa habari

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kutoa maudhui anuai ili kukidhi tamaduni na mahitaji ya rika tofauti. Pia wanatakiwa kutoa maudhui ya elimu na kutenga muda wa dakika tisini kwa ajili wa habari na matukio. Uzingatiaji wa uanuai wa vipindi kwa robo mwaka iliyotathminiwa unaoneshwa kwenye Jedwali 6.2.2a na Jedwali 6.2.2b.

### Jedwali 6.2.2a Uanuai wa vipindi vya televisheni

TV	Utofauti wa vipindi	Maudhui ya elimu	Uzingatiaji wa dakika tisini wa habari
ITV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
UTV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Tumaini TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
East Africa TV	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Star TV Tanzania	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC 1	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TV Imaan	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Arise and Shine	Haijakidhi	Haijakidhi	Imekidhi
WRM TV	Haijakidhi	Haijakidhi	Haijakidhi
Clouds TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Hope Channel Tanzania	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Upendo TV	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Mahaasin TV	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Channel Ten Plus	Haijakidhi	Haijakidhi	Haijakidhi
TVE	Haijakidhi	Haijakidhi	Haijakidhi

### Jedwali 6.2.2b Uanuai wa vipindi vya redio

Redio	Utofauti wa vipindi	Maudhui ya elimu	Uzingatiaji wa dakika tisini wa habari
Radio One	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC Taifa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Adventist World Radio (AWR)	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Clouds FM	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
East Africa Radio	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
EFM	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Wasafi FM	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
TBC International	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Radio Free Africa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Bongo FM	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Radio Maria	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi



### 6.2.3 Uzingatiaji wa maudhui ya ndani (local content)

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kuhakikisha kwamba asilimia 60 ya vipindi vyao vimetengenezwa ndani ya nchi, ili ikichagiza utamaduni, lugha, na maudhui ya ndani ya nchi. Matokeo ya upimaji ya uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwa robo mwaka yameoneshwa kwenye Jedwali 6.2.3a na Jedwali 6.2.3b hapa chini.

#### Jedwali 6.2.3a Uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya televisheni

TV	Yenye umuhimu kwa jamii	Lugha (Kiswahili au Kiingereza)	60% ya uzalishaji wa maudhui ya ndani
ITV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
UTV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Tumaini TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
East Africa TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Star TV Tanzania	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC 1	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TV Imaan	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Arise and Shine	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
WRM TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Clouds TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Hope Channel	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Upendo TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Mahaasin TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten Plus	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TVE	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi

#### Jedwali 6.2.3b Uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya redio

Redio	Yenye umuhimu kwa jamii	Lugha (Kiswahili au Kiingereza)	60% ya uzalishaji wa maudhui ya ndani
Radio One	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC Taifa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Adventist World Radio (AWR)	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Clouds FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
East Africa Radio	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
EFM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Wasafi FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC International	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Radio Free Africa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Bongo FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Radio Maria	Imekidhi	Haijakidhi	Imekidhi

Mamlaka ya mawasiliano Tanzania (TCRA) imechukua na itaendelea kuchukua hatua stahiki za kiudhibiti kwa watoa huduma wote walioshindwa kukidhi vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa kanuni husika.

### 6.3 Ubora wa huduma za Posta na Usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Vipimo vya ubora (Quality of Service - QoS) kwa watoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi (Domestic Couriers) katika kanda A (inter-town A), vilifanyika kuanzia Julai hadi Septemba 2024 kwa kuzingatia vigezo na mbinu za vipimo zilivyoainishwa kwenye Kanuni ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2018. Kanda A inahusisha mikoa inayofikika ndani ya siku moja kutoka Dar es Salaam.

Vipimo vilizingatia kasi ya huduma toka bidhaa inapokabidhiwa kwenye ofisi ya mtoa huduma hadi inapowasilishwa kwa mteja. Kigezo cha ufanisi kilizingatia angalau 85% ya bidhaa zote zilizotumwa ziwasilishwe kwa mteja ndani ya siku moja. Jedwali 6.3 linaonyesha matokeo ya upimaji iliyofanywa.

#### Jedwali 6.3 Ubora wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Mtoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi	Kasi ya uwasilishaji kwa eneo la kanda A
Air Tanzania	Imekidhi
Precision Air	Imekidhi
Tanz Movers	Imekidhi
Advanced Logistics	Imekidhi
Delex Courier & Logistics Limited	Imekidhi
Ellymo Company Limited	Imekidhi
Segax	Imekidhi
Geamos Co. Ltd	Haijakidhi
Marathon Logistics	Haijakidhi
Blaze	Haijakidhi
Mwanga Logistics	Haijakidhi
Sga Cash In Transit (T) Limited	Haijakidhi
Almko Investment Limited	Haijakidhi
Cmtl Group	Haijakidhi
Couriemate	Haijakidhi
Easy Movers	Haijakidhi
Jonz	Haijakidhi
Kleafast Couriers & Logistics	Haijakidhi
Simba Courier	Haijakidhi

Mamlaka ya mawasiliano Tanzania (TCRA) imechukua na itaendelea kuchukua hatua stahiki za kiudhibiti kwa watoa huduma wote walioshindwa kukidhi vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa kanuni husika.

## 6.4 Majaribio ya ulaghai

### Tanzania Bara

Mkoa	Airtel	Halotel	Tigo	TTCL	Vodacom	Jumla
Rukwa	1,582	428	1,523	1,247	791	5,571
Morogoro	902	15	2,880	34	1,655	5,486
Mbeya	252	70	326	368	96	1,112
Dar es Salaam	246	29	533	54	97	959
Arusha	94	5	84	15	153	351
Kilimanjaro	5	3	117	5	205	335
Pwani	108	3	95	7	9	222
Mwanza	42	6	95	25	46	214
Tabora	14	26	36	111	11	198
Katavi	0	34	16	83	58	191
Songwe	1	46	77	42	0	166
Dodoma	6	7	110	6	3	132
Iringa	5	3	98	10	2	118
Tanga	6	5	88	4	4	107
Kagera	13	5	65	0	12	95
Ruvuma	3	3	61	12	2	81
Shinyanga	5	6	31	18	11	71
Singida	1	0	51	13	2	67
Geita	0	2	52	8	3	65
Kigoma	13	3	18	21	5	60
Manyara	35	3	17	4	1	60
Njombe	0	1	19	29	1	50
Mtwara	2	2	33	3	1	41
Mara	1	4	31	1	3	40
Lindi	2	0	21	4	2	29
Simiyu	0	2	11	2	1	16

### Zanzibar

Mjini Magharibi	70	0	50	1	1	122
Kaskazini Pemba	0	0	15	0	0	15
Kaskazini Unguja	0	0	12	0	0	12
Kusini Pemba	0	0	10	0	0	10
Kusini Unguja	0	0	6	0	0	6
<b>Jumla</b>	<b>3,446</b>	<b>711</b>	<b>6,608</b>	<b>2,127</b>	<b>3,177</b>	<b>16,069</b>

Kielelezo hapo chini kinaonesha majaribio ya ulaghai kwa kila mtoa huduma kwa robo ya mwaka iliyoishia Juni 2024 na Septemba 2024. Tigo ilikuwa na idadi ya majaribio mengi zaidi ya watoa huduma wengine.

Robo ya mwaka inayoishia	Airtel	Halotel	Tigo	TTCL	Vodacom	Jumla
Juni 2024	6,069	469	10,242	2,093	3,384	22,257
Septemba 2024	3,446	711	6,608	2,127	3,177	16,069
Badiliko	-43%	52%	-35%	2%	-6%	-28%


Takwimu zinaonesha kuwa majaribio ya ulaghai kwa ujumla yamepungua kwa wastani wa 28%.

Chati 6.4a inaonesha majaribio ya ulaghai kimkoa. Mikoa ya Rukwa na Morogoro ndiyo inayoongoza, ikiwa na zaidi ya theluthi moja ya majaribio yote ya ulaghai nchini. Mbeya, Dar es Salaam na Arusha zinafuata kwa majaribio ya ulaghai kwa zaidi ya 1% hadi 10%.

Mikoa mingine ya Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na Kusini Pemba ina idadi ndogo ya majaribio. Kila mkoa ukirekodi 0.01%.

### Chati 6.4a Idadi majaribio ya ulaghai kimkoa kwa robo mwaka inayoishia Septemba 2024

#### Tanzania Bara



Rukwa na Morogoro ni mikoa inayoongoza kwa kuwa na zaidi ya robo tatu ya majaribio ya ulaghai

Mikoa ya Kaskazini Unguja, Kusini Pemba na Kusini Unguja ina idadi ndogo ya majaribio ya ulaghai

#### Zanzibar


Mjini Magharibi	122
Kaskazini Pemba	15
Kaskazini Unguja	12
Kusini Pemba	10
Kusini Unguja	6

## Jedwali 6.4 Majaribio ya ulaghai kiwilaya kwa mikoa minne inayoongoza

Mkoa	Wilaya	Majaribio ya Ulaghai
<b>Rukwa</b>	Sumbawanga	5198
	Nkasi	250
	Kalambo	122
<b>Morogoro</b>	Ifakara	3922
	Kilombero	1306
	Morogoro	127
	Kilosa	89
	Ulanga	21
	Mvomero	10
	Malinyi	8
	Gairo	3
<b>Mbeya</b>	Mbeya	993
	Mbarali	66
	Chunya	21
	Rungwe	21
	Kyela	11
<b>Dar es Salaam</b>	Ubungo	314
	Kinondoni	286
	Temeke	210
	Ilala	125
	Kigamboni	24

Mgawanyo wa asilimia ya majaribio ya ulaghai mtandaoni kwa kila mtoa huduma umeoneshwa katika Chati 6.4b.

Chati 6.4b Mgawanyo wa asilimia ya majaribio ya ulaghai mtandaoni kwa kila mtoa huduma



# 7. Idadi ya Leseni na Vyeti

7.1 Leseni		Mawasiliano ya simu na na Intaneti	
Aina ya leseni	Namba		
	Juni 2024	Septemba 2024	
Network Facilities Licences	34	35	
Network Services Licences	15	16	
Application Services Licences	142	146	
Aircraft Stations	169	176	
Amateur Stations	20	23	
Fixed VSAT Terminals	42	36	
Mobile VSAT Terminals	2	2	
Satellite Ground Earth Stations	1	1	
Ship Stations	35	36	
HF Radio Stations	23	21	
VHF- UHF Radio Repeaters	2	2	
VHF - UHF Radio Station with Pair of Frequency	118	109	
VHF - UHF Radio Station with Single Frequency	192	184	
Numbering	576	493	
Utangazaji			
Aina ya leseni	Namba		
	Juni 2024	Septemba 2024	
National Content Television (FTA) Licences	16	16	
District Content Television (FTA) Licences	23	22	
National Content Radio Licences	14	14	
Regional Content Radio Licences	31	33	
District Content Radio Licences	177	182	
Community Radios	15	17	
Community Televisions	-	-	
National Content Televisions by Subscription	25	28	
District Content Televisions by Subscription	1	1	
National Content (support services)	3	3	
Online Content Aggregators	5	6	
Weblogs (Blogs)	64	66	
Online Radios	9	10	
Online Televisions	215	210	
Cable Televisions	63	63	

Posta na watoa huduma ya usafirishaji		
Aina ya leseni	Namba	
	Juni 2024	Septemba 2024
International Courier	7	6
East Africa Courier	2	2
Intercity Transporters	71	76
Intracity Courier	18	16
Public Postal	1	1
Domestic Courier	47	47

## 7.2 Vyeti

Aina ya leseni	Idadi	
	Juni 2024	Septemba 2024
Global Maritime Distress and Safety Systems	152	177
Type Approval	4,590	4,774
Registration for Satellite Mobile Phones	32	32

---

## 8. Hitimisho

Hali ya mawasiliano katika robo inayoishia Septemba 2024 imeonesha maendeleo makubwa kwa kuongezeka kwa matumizi ya huduma za mawasiliano, yakichochea na ushindani endelevu katika kutoa huduma hizo. Moingoni mwa mafanikio hayo ni kuenea kwa mtandao wa simu za mkononi kwa teknolojia mbalimbali, ambapo mtandao wa 3G umeenea kufikia asilimia 90 ya watu, na hivyo kuwezesha upatikanaji wa huduma ya Intaneti.

Aidha, kuenea kwa mtandao wa 4G kufikia asilimia 85 ya watu kumeongeza kasi na upatikanaji wa uhakika wa huduma za mawasiliano. Wakati huo huo, mtandao wa 5G umeenea kufikia asilimia 18 ya watu huku ukiongeza kasi ya Intaneti ambayo ni muhimu katika kuwezesha sekta za kijamii na kiuchumi. Mafanikio hayo yameambatana na uboreshaji wa huduma za mawasiliano, usimamizi ulioimarika wa usalama mtandaoni na uimarishaji wa miundombinu unaowezesha ukuaji wa uchumi wa kidijiti.

Vilevile sekta ya utangazaji imeonyesha mwelekeo mzuri ambapo redio za FM zimefikia asilimia 78 ya watu na huduma za utangazaji za televisheni kwa kutumia mitambo ya ardhini (DTT) imefikia asilimia 58 ya watu. Ukuaji huu unaonyesha mabadiliko ya kasi ya sekta hii katika kukabiliana na mahitaji ya watumiaji. Aidha, maboresho katika sekta yamewezesha jamii kupata habari kwa muda na hivyo kuwezesha shughuli za kijamii na kiuchumi.





Mwasiliano Towers,  
20 Sam Nujoma Road,  
14414 Dar es Salaam, Tanzania.  
Email: dg@tcra.go.tz

 @tcra\_tanzania

